

# CHUO KIKUU CHA SOKOINE CHA KILIMO

## CHAMA CHA WANATALUMA (SUASA)



### ZABUNI YA KUKODI CHUMBA KWA AJILI YA BIASHARA

Chama cha wanataaluma wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUASA) kinakaribisha zabuni kutoka kwa watu wenye nia na uwezo kukodi / kupanga Chumba kimoja kilichopo katika eneo la SUASA Club iliyoko Kampasi Kuu ya SUA. Kinaweza kutumika kwa shughuli za aina mbalimbali isipokuwa uuzaji wa vinywaji na vyakula vilivyopikwa. Chumba kina ukubwa wa takribani “Square metre” 10 na baraza lenye ukubwa wa takribani “Square metre” 30. Chumba kipo katika jengo lililopo SUASA Club upande wa barabarani.

#### SIFA ZA MWOMBAJI

1. Awe na uthibitisho wa kutambuliwa kisheria na mamlaka husika
2. Awe na uthibitisho wa kuwa mlipa kodi mwaminifu
3. Awe na uzoefu unaothibitika wa kuendesha biashara husika
4. Awe na leseni hai ya kuendesha biashara husika

#### MASHART YA ZABUNI

1. Mwombaji anatakiwa kununua nyaraka za zabuni zenye maelezo ya kina ya mahitaji ya zabuni hii iliyotangazwa kwa kulipa ada ya Tsh 50,000/= (Elfu Hamsini tu) taslimu kwenye akaunti namba 0152079421201-SUASA Benki ya CRDB, SUA fedha ambayo haitarejeshwa. Nyaraka zenye maelezo ya kina ya zabuni zinapatikana katika ofisi ya SUASA chumba namba 340 Kampasi Kuu, SUA. Nyaraka zitatolewa kwa aliyethibitisha kufanya malipo tajwa hapo juu.
2. Mwombaji anaruhusiwa kutembelea Chumba kilichopo SUASA Club katika Kampasi Kuu siku za kazi kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni. Mwombaji anashauriwa kuonana na uongozi wa SUASA ili kuona chumba husika. Pia mwombaji anashauriwa kuwasiliana na wahusika;

ambao namba zao zimeambatanishwa kwenye tangazo hili mara atakapohitaji maelezo mengineyo kuhusu zabuni hii.

3. Siku ya mwisho ya kuleta zabuni itakuwa tarehe 27 Machi, 2017 saa 8:00 Mchana. Maombi yatakayowasilishwa baada ya muda wa zabuni kuisha hayatapokelewa .
  
4. Maombi ya zabuni yawekwe kwenye bahasha. Bahasha iandikwe “ ZABUNI YA KUKODI CHUMBA,MWENYEKITI WA SUASA, S.L.P 3000, MOROGORO” na kufungwa kwa lakiri yapelekwe Chumba namba 340, jengo la utawala SUA, Kampasi Kuu.
  
5. Zabuni zitafunguliwa mbele ya wazabuni wote walioomba au wawakilishi wao watakao amua kuhudhuria kwenye ufunguzi huo tarehe 27 Machi 2017 Saa 8:30 Mchana katika ukumbi wa Baraza la Chuo jengo la Utawala

**Wasiliana kwa mwongozo Zaidi na:-**

1. Mwenyekiti SUASA-0752 562240
2. Katibu SUASA-0754477486
3. Mhazini SUASA 0655 441 788
4. Mwenyekiti kamati ya uendeshaji wa SUASA CLUB-0689 650 296